BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUMU ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

MEI, 2025

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuweza kutujaalia uhai na afya njema vilivyotuwezesha kukutana hapa kwa lengo la kujadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yetu Tukufu kwa mwaka 2025/2026. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kutumia hekma, busara na weledi wa hali ya juu katika kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inatumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zake za kuimarisha miundombinu na maslahi ya Wizara hii kupitia wapiganaji wote wa Idara maalumu. Uongozi wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu na ari Rais wetu mpendwa kuwathamini na kuwapa nguvu Wakuu wa Idara hizi ili wazidishe juhudi za kusimamia vyema majukumu waliyopewa.

**Mheshimiwa Spika:** Pia, napenda kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza hili, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka

*2024* zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika:** Aidha, niwapongeze na kuwashukuru viongozi wa Ofisi hii wakiongozwa na Waziri hodari na mchapakazi Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed, Katibu Mkuu wake ndugu Issa Mahfoudh Haji na Afisa Mdhamini Pemba ndugu Thabit Othman Abdallah. Aidha, niwapongeze Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya, Makamanda wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ na watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu na kuchangia kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa umuhimu wake, naomba kutumia nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na maagizo ya Kamati pamoja na kusimamia kwa ukamilifu mipango ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Bajeti ya mwaka *2024/2025*, jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya Kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio mapya ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka *2025/2026* ili yapate baraka za Wajumbe wako na kwa muktadha huo, tunaliomba Baraza lako tukufu liridhie na liipitishe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa namna ya pekee, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tulipoipitia bajeti hii, kwa kuonesha umahiri na mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu waliyopangiwa.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambulisha wajumbe wa kamati hii kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| *3.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Jamal Kassim Ali | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Haji Shaaban Wazir | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *10.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika:** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia vyema nafasi yake katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha na programu zote zilizopangwa kufanyiwa kazi kupitia Mafungu ya Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2024*.

**Mheshimiwa Spika:** Ni imani ya Kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizokadiriwa kutumika katika Ofisi hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo yao katika kipindi husika ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi mbali mbali ya kimaendeleo inayotekelezwa kwa madhumuni ya ilivyoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa kuanza na Programu za Makao Makuu **[Fungu D 01].** Kupitia Programu Kuu ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;** Kamati imebaini kuwepo kwa kiwango kidogo cha mapato kilichokusanywa kupitia vyanzo vya mapato kwa baadhi ya Halmashauri za Mabaraza ya Miji na Manispaa ambapo imeelezwa kuwa uhaba wa vyanzo vya mapato na vifaa vya kisasa ni njia moja wapo iliyopelekea kupungua kwa mapato hayo. Katika suala hili, Kamati kupitia mafungu ya Mikoa imegundua kwamba baadhi ya Mikoa ilipangiwa kukusanya kiwango kikubwa cha mapato bila kuangalia uwezo wa vyanzo vya mkoa husika pamoja na nguvu ndogo ya ukusanyaji wa mapato kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa. Kamati katika ziara zake za kawaida ilitembelea baadhi ya Mabaraza ya Miji na Manispaa na kuona juhudi zao za ukusanyaji wa mapato ambapo kimsingi haziridhishi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Taasisi hizi kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato

kwa kuepuka kuoneana muhali katika kazi zao pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya ulipaji wa tozo na ada kwa hiari ili kuongeza kasi ya mapato kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika:** Katika programu ndogo **[SD010102]** ya **Uratibu wa Serikali za Mitaa** yenye lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji na upatikanaji wa huduma za kijamii. Kamati yangu inapata mashaka kwamba lengo la programu hii halitofikiwa kutokana na changamoto za vifaa ambazo zinazikabili Halmashauri zetu, kwa mfano Manispaa ya Chake–Chake, Manispaa ya Kaskazini A na Baraza la Mji Wete kwa pamoja wanakabiliwa na changamoto ya gari za kuzolea taka. Ukosefu huu unazifanya taasisi hizi kushindwa kufikia malengo katika jukumu la usafi na hivyo kuwa na nguvu ndogo ya kuweka miji yetu safi na kuchangia miji hii kutokuwa na haiba nzuri siku hadi siku. Pamoja na hayo, kamati imeelezwa kuwepo kwa mpango wa ununuzi wa gari ishirini na tisa (29) ambayo yatasambazwa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mpango huu ni mzuri na utakapokamilika utaleta ufanisi kwa Halmashauri hizi.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati imepata ukakasi kwa upande wa Fungu D01 la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia kifungu kidogo cha Mapato cha D0104 kinachohusu Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati wakati ikipitisha bajeti hii ilipokea taarifa mbili juu ya mapato ya Tsh. Bilioni Moja na Milioni Mia Nane (Tsh. 1,800,000,000) yanayotakiwa kukusanywa kwenye usajili na leseni. Tunaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango watoe taarifa rasmi juu ya mapato hayo kwani itakumbukwa kuwa kwa miaka kadhaa iliyopita fungu hili halikuonekana wazi na lilisomeka ndani ya Fungu hili la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika:** kupitia programu ndogo ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa** iliyokusudiwa kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya Mikoa ili hatima yake iweze kuongeza kasi ya utawala wa sheria na ushirikishwaji wa wananchi katika nyanja za kiuchumi na kijamii. Kwa kuwa programu hii inatarajiwa kufikia malengo hayo, kamati yangu inaishauri Serikali kuharakisha mpango wa ujenzi wa ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutokana na changamoto kubwa ya majengo ya ofisi au kuwa na ofisi ambazo haziendani na hali halisi ya sasa.

**Mheshimiwa Spika:** kama tunavyofahamu kuwa afisi ya Afisa Mdhamini Pemba ni kiungo muhimu katika uratibu wa shughuli za Serikali kwa upande wa Pemba kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kamati haina mashaka na utekelezaji wa programu za ofisi hii kama zilivyopangwa kupitia programu kuu ya [PD0104] ya uendeshaji na Uratibu wa Ofisi. Aidha, kamati imebaini kuwa ofisi ya Afisa Mdhamini ina eneo la kutosha na mikakati imara ambayo itasaidia kupata jengo lake jipya la ofisi lenye kukidhi mahitaji ya muda mrefu. Kwa mantiki hiyo, kamati inaishauri Serikali kupitia mpango wake wa majengo mapya ya ofisi na afisi ya Afisa Mdhamini Pemba kupewa kipaumbele katika kupatiwa jengo jipya na la kisasa.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati wakati ikifuatilia utekelezaji wa kazi za bajeti, ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi ya Mrajis wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGO's) kwa Unguja na Pemba na kuridhika na utendaji bora wa kazi wanaofanya kwa maslahi ya nchi yetu. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuona Ofisi hii inatatizo la ufunyu wa nafasi hali iliyopelekea wafanyakazi wote wa taasisi hiyo kufanya kazi katika chumba kimoja. Kutokana na kuliona hili, kupitia Programu ndogo ya SD010404 ya shughuli za Uratib Utekelezaji wa Jumuiya zisizo za kiserikali tunaishauri Serikali iwapatie jengo jengine lenye nafasi ya kutosha ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06):

**Mheshimiwa Spika:** Kwa upande wa programu za Idara Maalum za SMZ ambazo programu yake kuu **[PD0102]** Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum inatekelezwa kupitia **fungu D01** la Ofisi Kuu kwa lengo la kuweka uwiano wa Idara zote za SMZ katika masuala ya kiutawala. Kamati imeridhika na kazi nzuri za wapiganaji wetu wa vikosi vya SMZ kwa kushirikiana na vikosi vya SMT kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao kwa msingi wa kudumisha amani kwa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika:** kamati inaishauri Serikali kuendelea na mradi wa miundombinu ya barabara zilizoingia kwenye makambi ya Idara Maalum ikiwemo barabara ya

kikosi cha KVZ Muyuni na barabara ya JKU Dunga. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu maalumu ambao utasaidia vikosi vyetu baada ya kukamilisha miradi ya ujenzi wa mahanga na nyumba za maafisa kupatiwa samani (furniture) ambazo zitaondoa usumbufu wa matumizi wa nyumba hizo pamoja na ofisi zake. Tatizo la samani inaonekana katika vikosi vyote ambavyo vimekamilisha ujenzi katika kambi zake.

**Mheshmiwa Spika:** Kwa upande mwengine Kamati inakisikitishwa na kitendo cha muwekezaji wa kilimo cha miwa ambaye anafanya kazi kwa ushirikiano na Jeshi la Kujenga Uchumi na Idara ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar. Matarajio ya idara hizi ni kupata faida kupitia kilimo cha miwa ambacho wamewekeza nguvu kubwa katika uzalishaji wake bila ya kupata mafanikio kama walivyotarajia kutokana na changamoto za muwekezaji.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa msingi huo, kamati inazishauri Idara hizi kuandaa programu zao wenyewe ambazo zitawekeza kwenye rasilimali fedha na rasiliamli watu kwa lengo la kuepuka kadhia ya kushuka kiwango cha faida baada ya mavuno kutokana na makato makubwa wanayofanyiwa na muwekezaji. Sambamba na upatikanaji wa wataalamu wa kilimo ambao kwa kiasi kikubwa ndio watakao sababisha maendeleo ya kilimo na mifugo kwa idara hizi. Aidha, kamati inaishauri Wizara kukamilisha mradi wa ufugaji kuku katika kambi ya Chuo cha Mafunzo Hanyegwa Mchana kutokana na kusimama kwa muda mrefu ambapo ujenzi wa miundombinu ulianza na kuachwa njiani.

**Mheshimiwa Spika:** kimsingi inazipongeza kampuni za ujenzi za Idara Maalum kutokana na kazi kubwa na nzuri wanazozifanya kila siku. Mfano mzuri ni Kikosi cha KMKM katika ujenzi wa Mahakama Jumuishi Chake – Chake Pemba ambayo ujenzi wake upo katika hatua ya kuridhisha sana tofauti na mkandarasi wa mwanzo ambaye alishindwa kuendeleza ujenzi huo kwa wakati waliokubaliana. Aidha, pongezi za ujumla ziende kwa kampuni ya JKU, KVZ na Chuo cha Mafunzo kwa kuaminiwa na Serikali kutokana na kazi zao bora na za kisasa ambazo wamekuwa wakizitekeleza kwenye miradi ya kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika:** Wakala wa Ulinzi wa JKU umeanzishwa rasmi kwa sheria namba 2 ya mwaka 2015 ukiwa na malengo ya kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii ili kukuza uchumi wan chi pamoja na kuhakikisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za ulinzi wa uhakika na uliobora. Aidha, wakala huu unakabiliwa na changmoto ya afisi yake ya kudumu jambo ambalo linakwaza utendaji wao wa kazi.

**Mheshimiwa Spika:** kwa mara nyengine tena Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka 2025/2026 inajenga jengo la Utawala kwa Wakala wa Ulinzi JKU kwa vile Wakala huo umekabiliwa na tatizo kubwa la afisi. Aidha Kamati inampongeza Mkurugenzi wa Wakala wa Ulinzi wa JKU kwa kusimamia vyema Mapato ya Wakala huo na kuweza kuchangia Serikali Tsh. Milioni Mia Nane (Tsh. 800,000,000). Pamoja na pongezi hizo, kamati bado inazitaka taasisi za Serikali zinazodaiwa na Wakala huo kulipa deni lao lote wanalodaiwa kwa muda mrefu sasa, kwani hadi tunapokea taarifa ya utekelezaji ya Wakala kwa kipindi cha miezi tisa (Julai hadi Machi 2024/2025) Wakala huo unazidai Taasisi mbali mbali za SMZ kiasi cha takriban Tsh. Bilioni tatu (Tsh. 3,000,000,000) na hivyo kuwa changamoto kubwa katika ukusanyaji wao wa mapato.

**Mheshimiwa Spika:** vile vile, kamati inatoa pongezi kwa marekebisho ya sheria ya KMKM namba 3 ya mwaka 2003 ambayo imerekebishwa mwaka 2024 na sasa kuwafanya washiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali kupitia miradi ya kiuchumi. Sambamba na marekebisho ya sheria ya Kikosi cha Valantia Zanzibar sheria Namba 5 ya mwaka 2004 ambayo marekebisho yake yameipa idara hii kuwa nguvu katika shughuli za kibiashara. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kusimamia kikamilifu kukamilika kwa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ ambayo mchakato wake umeanza na kufikia hatua ya kujadiliwa na makatibu wakuu.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12)

**Mheshimiwa Spika:** ni jambo la faraja kuona Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio

ya Kijamii imezidisha kasi ya utekelezaji kwa mafanikio makubwa ya programu kuu ya **Kusajili vizazi, vifo na Kadi za Utambulisho;** kwa lengo la kuimarisha huduma za usajili kwa ufanisi na kutoa vyeti pamoja na vitambulisho kwa wakati. Kupitia hotuba hii Kamati inaipongeza Wakala kwa juhudi zake za utoaji vyeti kwa njia rahisi na ya haraka ambayo kwa kiasi kikubwa imepunguza tatizo la ucheleweshaji wa vyeti na hivyo, kuwapunguzia wananchi usumbufu na kuimarisha udhibiti wa taarifa za matukio ya kijamii. Sambamba na hayo, kamati inashauri Serikali kuwapatia fedha za kutosha Wakala wa Usajali wa Matukio ya Kijamii ili kujiendesha programu hii bila ya uwepo wa changamoto za vifaa.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inaishauri Serikali kuipatia fedha Taasisi hii kwa dhumuni la kupata mahitaji yake ya msingi kama vile samani (viti, meza, makabati kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka na kumbukambu zao) za ofisi pamoja na kuweza kulipa maposho ya muda wa baada ya saa za kazi. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuja na mradi maalumu wa ujenzi wa ofisi mpya za wakala zenye nafasi ya kutosha na utaoimarisha zile zilizopo ili kwenda sambamba na mahitaji ya sasa na ya baadae.

HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika:** Naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu na niwashukuru pia, Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao na uzalendo wao kwa mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Sambamba na hilo, Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kupitia wizara hii kwa uamuzi wake wa kuendeleza mradi wa ujenzi wa ofisi za Masheha kwa upande wa Unguja na Pemba kwa lengo la kukuza na kuimarisha utawala bora nchini pamoja na kuzitaka Idara Maalumu kuibua miradi mbalimbali ya kimaendeleo ambayo ina lengo kupunguza changamoto ya fedha za matumizi.

**Mheshimiwa Spika:** Mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishe Bajeti hii na hatimae

waidhinishe makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wote wa 2025/2026 kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa heshima na taadhima na kwa niaba kamati yangu *Naunga Mkono Hoja na Naomba Kuwasilisha.*

……………………………….

**(Mhe. Machano Othman Said)**

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**